GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

Mapenzi Yangu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZU NO. 242 **M/haram-Safar** 1446 **AH** **Agosti–** 2024 **Zahoor** 1403 **HS** **BEI TSH 800/=**

Wasiyyat

Wasiyyat.

TOLEO LA KWANZA.

Kutokana na umuhimu mkubwa wa kutoa elimu na mafunzo ya mambo mbalimbali yanayohusu Mpango wa Wasiyyat, Idara ya Wasiyyat taifa imeonelea kuwa ni muhimu kuleta mbele ya Wanajamaat tafsiri ya Maswali yanayoulizwa mara kwa mara kuhusiana na Nizam ya Wasiyyat yaliyoandaliwa na Idara ya Wasiyyat ya nchi ya **USA** (Marekani).

Makala hii ya maswali itaendelea kuwasilishwa kwa wasomaji hatua kwa hatua ili kujenga uelewa mpana na kupata utatuzi wa maswali mengi yanayoulizwa kuhusiana na Mpango wa Wasiyyat.

UK. 05

Kwa Mawasiliano na Maoni kuhusu Nizam ya Wasiyyat
PIGA: 0688 094211-Katibu wa Wasiyyat Taifa

Mjue Jinni

Sehemu ya Tatu.

UK. 3

Jalsa Salana UK Yatikisa



Kwa kiwango chochote utakachokitumia, Jalsa Salana ya 54 ya uingereza ambayo kwa hivi sasa imevaa koti la Jalsa Salana ya kimataifa ilikuwa ni ya mafanikio makubwa. Ni dhihirisho jingine la msaada mwingine wa Allah kwa wafuasi wa Masih Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] ambaye ni mtumishi mtiifu wa Mtukufu Mtume

UK. 09

ANGUKO LA MTU LIPO KWENYE KILELE CHA MAFANIKIO YAKE >UK .10

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

UTAFITI

Utamaduni wa utafiti umetupiga chenga katika Afrika. Jazba, ari, mshawasha vyote hivi havipatikani katika uwanja wa utafiti, na upungufu huu umetuletea madhila makubwa. Kila kitu tunachokiona basi tunaona kipo tu na hatujisumbui kufahamu chimbuko lake, faida na hasara ya kitu hicho.

Twende kwa mfano, wangapi tunajisumbua kufahamu jina la ukoo, je lilitokana na nini? Na maana yake hasa ni nini? Kabila lake limetokea wapi na limefikaje lilipo? Kijiji anapoishi kimepataje jina lake, wilaya, Mkoa, nchi, bara lako la Afrika limepata jina hili limetoka wapi? Lina maana gani? Utamaduni huu kimsingi ni lazima uanze na kuimarishwa kwenye familia. Wazazi wanao wajibu wa awali wa kujenga na kuimarisha utamaduni huu.

Kukosekana kwa utamaduni huu kumeigharimu Afrika, Nchi nyingine kwa mathalani Merikani inatumia fedha nyingi katika utafiti kuliko nchi yoyote nyingine Duniani. Tizama hatua waliyopiga na huku Afrika tafiti zinazofanywa ni zile zinazofanywa kwa kufadhiliwa na mataifa hayo ambayo maendeleo yao, uhai wao ni kutunyonya na kutudumaza. Tafiti wanazogharamia ni zile ambazo zinasaidia kuendelea kutunyonya na kutufunga kwenye minyororo ya kuendelea kunyonya rasilimali zetu.

Ni kujidanganya kufikiri ya kwamba nchi hizo zinaweza kuwa na jema lolote kwa ajili yetu. Mwamba ngoma huvutia kwake! Na kazi hiyo wanaijua, wanatoa msaada pale tu ambapo wanaelewa tutaendelea kuumia na tutaendelea kuwapigia magoti na huku tukiwa na bakuli mikononi, tukilia saidia masikini!

Kama kweli tunataka ukombozi wetu wa pili wa bara la Afrika ni lazima yatokee mapinduzi ya fikra. Hakuna atakayetuletea Maendeleo. Ukiendelea akale wapi? Hilo ni kulizingatia na kulitia maanani. Allah Ametujaalia utajiri mkubwa katika Afrika. Inasikitisha ya kwamba sisi ni watu tulio mtoni lakini tunalia ya kwamba hatuna maji ya kunywa, ni msiba wa kutoona, Tubadilike.

Tujenge utamaduni wa kufanya utafiti, tuelewe chanzo cha maafa yetu. Lini mvua ya balaa ilianza kutunyeshea na ndipo tutajua ni wakati gani nguo zetu zitakapokauka. Kulinusuru Bara letu tunashauri zichukuliwe hatua zifuatazo:-

•Tujenge utamaduni wa utafiti toka kiwango cha familia hadi juu.


•Serikali zetu ziweke pesa za kutosha katika utafiti na wala wasisubiri msaada kutoka nje.

•Panapohitajika utafiti tunapafahamu sisi sio mtu mwingine kutoka nje. Uchungu wa mwana aujuae mzazi. Tusisubiri asilani mtaalamu kutoka mahali popote kutuonesha njia-kitanda usichokilalia huwezi kufahamu kunguni wake wanavyoshambulia.

•Tafiti zikishafanywa zisiwekwe kwenye sanduku la sahau. Zitizamwe na zitumike iwapo ni za manufaa kwa jamii.

•Zawadi zitolewe kwa utafiti aliyeibua jambo la manufaa kwa jamii.

•Shule zetu za Msingi, Sekondari na vyuo vikuu ziwe chemchem ya utafiti kwani kama walivyosema wahenga wetu. ***"Samaki mkunje angali mbichi"***.




QUR'AN TUKUFU

Surah 24:34

"Na washike utawa wale wasiopata kuoa mpaka Mwenyezi Mungu Awatajirishe katika fadhili Zake. Na wale wanaotaka hati katika wale inayowamiliki mikono yenu ya kuume, basi waandikieni, kama mkiona wema kwao. Na wapeni katika mali ya Mwenyezi Mungu Aliyowapeni. WALA MSIWASHURUTISHE VIJANA WENU WA KIKE KUFANYA UKAHABA KAMA WAKITAKA KUKAA UTAWANI, ILI KUTAFUTA VIFAA VYA MAISHA YA DUNIA. Na Atakayewashurutisha, basi hakika Mwenyezi Mungu baada ya kushurutishwa kwao ni Msamehevu, Mrehemevu."

وَلْيَسْتَعْفِفِ ٱلَّذِينَ لَا يَجِدُونَ نِكَاحًا حَتَّىٰ {
يُغْنِيَهُمُ ٱللَّهُ مِن فَضْلِهِۦ ۗ وَٱلَّذِينَ يَبْتَغُونَ ٱلْكِتَـٰبَ
مِمَّا مَلَكَتْ أَيْمَـٰنُكُمْ فَكَاتِبُوهُمْ إِنْ عَلِمْتُمْ فِيهِمْ
ۖ وَءَاتُوهُم مِّن مَّالِ ٱللَّهِ ٱلَّذِىٓ ءَاتَىٰكُمْ ۚ وَلَا خَيْر
ا تُكْرِهُوا۟ فَتَيَـٰتِكُمْ عَلَى ٱلْبِغَآءِ إِنْ أَرَدْنَ تَحَصُّن
لِّتَبْتَغُوا۟ عَرَضَ ٱلْحَيَوٰةِ ٱلدُّنْيَا ۚ وَمَن يُكْرِههُّنَّ فَإِنَّ
{ ٱللَّهَ مِنۢ بَعْدِ إِكْرَٰهِهِنَّ غَفُور رَّحِيم

[سُورَةُ النُّورِ: ٣٤]



NUKUU YA HADITHI

Abu Mas'ud Badri[ra] anasimulia ya kuwa: "Mtume (SAW) alihara-misha kutumia mapato yatokanayo na mauzo ya mbwa: NA MAPATO YA MWANAMKE MZINIFU na ada za watabiri na wapiga ramli." **(Bukhari na Muslim)**



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Masih Mau'udi a.s anasema: "Njia ya Zinaa ni mbaya sana, yaani INAZUIA KUFIKIA KWENYE LENGO LILILOKUSUDIWA na ni HATARI SANA KWA HATIMA YENU..." (Hekima ya Mafundisho ya Kiislamu, Ruhani Khazain, J. 10, uk.

Imeandaliwa na Musa
Salum 0717504690

Mola wetu, tumedhulumu nafsi zetu; na kama Hutusamehe na kuturehemu, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wenye hasara. Aamin

BODI YA UHARIRI

Msimamizi:	Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri:	Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta:	Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji:	Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji:	Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:	1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga 2. Mahmood Hamsin Mubiru. 3. Jamil Mwanga. 4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

Mjue Jinni

Kutoka Uk 01..

Sasa tunapoyatazama pia Maneno ya Mwenyezi Mungu, tunaambiwa kuhusu fitna tatu kubwa. Kwanza katika Surah Fatihah tunaomba

صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ

Enyi waaminio wa imam Mahdi a.s tuki talii Quran tuna kuta katika sura ya kwanza kabisa viashiria vya Dajjali vina tajwa na MwenyeziMungu.

Njia ya wale uliowaneemesha, ambao hawakughadhibikiwa na ambao hawakupotea. (Sura ya 1 aya ya 7

Aya hizi zina eleza pamoja na maovu ya Mayahudi na Wakristo pia tunamuomba Mwenyezi Mungu atuepushe na uwongo huo. Sasa fitna kubwa kabisa kwa mujibu wa Qur-an imeelezwa wazi kuwa ni kitendo cha kudai Mwenyezi Mungu ana mtoto, Mungu apishe mbali.

Mwenyezi Mungu Anasema

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَنُ وَلَدًا {89} لَقَدْ جِئْتُمْ شَيْئًا إِدًّا: {90} تَكَادُ السَّمَاوَاتُ يَتَفَطَّرْنَ مِنْهُ وَتَنشَقُّ الْأَرْضُ {وَتَخِرُّ الْجِبَالُ هَدًّا {91}} ن دَعَوْا لِلرَّحْمَنِ وَلَدًا {92

Nao husema: Rahmani Amejipangia mwana. Bila shaka mmeleta jambo lichukizalo. Karibu mbingu zitatuke kwalo na ardhi ipasuke na milima ianguke vipande vipande. kwa sababu wamemdaia Rahmani kuwa na mwana.(Sura ya 19 aya ya 89-92)

Mwenyezi Mungu ameweka wazi katika Qur'ani Tukufu kwamba kamwe Isa bin Maryam a.s hakuwahi kudai kuwa yeye ni Mungu au mwana wa Mungu au kuwaambia watu wamwabudu. Kwa kweli hili linathibitishwa na biblia yenyewe pia. Kauli na imani kama hizi za Isa bin Maryam a.s kuwa Mungu kunaweza tu kunasibishwa na Mpinga Kristo badala ya Isa a.s mwenyewe. Qur'an haitaji jina la Dajjal au mpinga kristo, hata hivyo inatuonyesha kwa uwazi maana halisi ya Dajjal na Dajjal mkubwa ni Mapadre wa Kikristo. Ushahidi mwingine wa wazi unaotuonyesha kwamba Dajjal mkubwa kwa hakika ni makasisi wa Kikristo, ushahidi huo ni Hadith zinazosema kwamba Masihi Aliye ahidiwa atavunja msalaba.

Ni nadra sana ambapo Mtukufu Mtume s.a.w anataja kuuawa kwa dajjal kwa kulinganisha na kuvunjika kwa msalaba. Kila Wakati ujio wa Masihi na Mahdi unapotajwa na kazi zake pia hitajwa, na kazi yake kuu ni kuvunja msalaba. Hadithi zinasema kwamba Dajjal atakuwa ndiyo fitna kubwa zaidi na atakuwa mwenye nguvu zaidi duniani.

Lakini hadithi nyingi pia zinatuonyesha kwamba Msalaba utakuwa ukitawala ulimwengu wakati wa Masihi, ndiyo maana Hadith zinasema

حَدَّثَنَا عَلِيُّ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ، حَدَّثَنَا سُفْيَانُ، حَدَّثَنَا الزُّهْرِيُّ، قَالَ أَخْبَرَنِي سَعِيدُ بْنُ الْمُسَيَّبِ، سَمِعَ أَبَا هُرَيْرَةَ ـ رضى الله عنه ـ عَنْ رَسُولِ اللهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ

" لَا تَقُومُ السَّاعَةُ حَتَّى يَنزِلَ فِيكُمُ ابْنُ مَرْيَمَ حَكَمًا مُقْسِطًا، فَيَكْسِرَ الصَّلِيبَ، وَيَقْتُلَ الْخِنزِيرَ، وَيَضَعَ الْجِزْيَةَ، وَيَفِيضَ الْمَالُ حَتَّى لَا يَقْبَلَهُ أَحَدٌ".

Mtume (s.a.w) amesema: “Haitasimama Saa mpaka ashuke mwana wa Maryamu kama hakimu muadilifu kati yenu, naye atauvunja msalaba, atauwa nguruwe, na atafuta ushuru wa Jizya. (Sahih Bukhari Hadithi namba 2476).

Ni nguvu moja tu inayoweza kutawala ulimwengu kwa wakati mmoja na haiwezekani kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w) ajipinge mwenyewe katika ahadithi hizi zote sahihi. Ukweli wa yeye kutuonyesha kwamba Msalaba na Dajjal wangetawala ulimwengu kwa wakati mmoja unaonyesha kwamba wanafanana na wana maana sawa nyuma yao.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s anasema: "Dajjal kwa kweli si mwingine bali ni watu wanaojulikana kama wamishenari wa Kikristo na wanafalsafa wa Kizungu. Wanakuwa kama taya mbili za Dajjal Aliyeahidiwa ambazo anakula nazo imani za watu kama chatu [yaani kuzimeza kwa nguvu aliyo nayo]. Kwanza ni watu wa kawaida na wajinga wanaonaswa ndani ya hatari hii. Hila za wamisionari; na kisha, wale wanaokwepa makucha yao wakichukizwa na imani chafu na za uwongo, wananaswa kwenye wavu wa mateso.

Kisha wanafalsafa wa Ulaya wanao endele kupinga uwepo wa mungu nao ni Dajjali. Ninaona kwamba watu wa kawaida wamo hatarini zaidi kwa uongo wa makasisi, pia wale wenye akili wanaathiriwa zaidi na uwongo unaoenezwa na wanafalsafa wa kizungu.” (Kitab-ul-Bariyyah, Ruhani Khazain, Juzuu 13, Ukurasa 252-253; maelezo ya chini)

Na: "Kumekuwa na Dajjal wengi na wanaweza kuongezeka na wengine zaidi. Lakini Dajjal mkubwa zaidi, ambaye udanganyifu wake ni mbaya sana katika makadirio ya Mwenyezi Mungu kwamba mbingu inaweza kupasuliwa kwaiyo, ni kundi linalomfanya mwanadamu kuwa Mungu. Imefafanuliwa vizuri ndani ya Qur'ani Tukufu aina mbalimbali za ghilba zinazofanywa na Mayahudi, Washirikina na wengineo, lakini haibagui [yaani hila] za kitu chochote ambacho kinaweza kusababisha mbingu kupasuka. Maana wayahudi ndio waanzilishi wa kusema Allah ana motto [Na wayahudi walipo sema Uzeir ni mwana wa Mungu.sura ya 9:30].

Hivyo na yule aliyeteuliwa na Mwenyezi Mungu katika Neno Lake Takatifu [ambaye ndiye Issa]. Na itakuwa ni dhuluma na ukatili mkubwa zaidi kujaribu kumtafuta mtu mwingine kama Dajjal mkuu kama sio hawa makasisi. Kwa vyovyote vile hatuwezi kuhalalisha kuwepo kwa Dajjal mkuu kuliko makasisi wa Kikristo wa siku hizi.

Ingawa Mwenyezi Mungu amewateua katika Neno Lake Takatifu kama Dajjal mkubwa zaidi. Dajjal kama huyo, Mwenyezi Mungu Mtukufu, Ambaye elimu Yake inayajua yaliyopita ya sasa na yajayo,angewezaje kumteua yeye kama sio watu hawa kuwa Dajjal mkubwa.

Alama ya Dajjal mkuu, ambayo inatuweka wazi zaidi ni hii tu kuwa ATAVUNJA MSALABA ambayo imedokezwa kutoka kwenye kitabu cha Hadithi sahihi Bukhari. Ni kwamba Dajjal mkuu atamuabudu Yesu na atahusisha wokovu na msalaba. Ni jambo la kufurahisha sana kwa wenye elimu kwamba katika nukta hii aya za uhakika za Qur'ani Tukufu na Ahadith sahihi zote zinaafikiana. Hivyo, ukweli kuhusu suala hili lenye utata limedhihirika au kufichuka kabisa. Qur'ani Tukufu inawataja waziwazi makasisi wa Kikristo kama Dajjal mkubwa zaidi na inautaja uwongo wao kuwa mkubwa kiasi cha kuangamiza mbingu na ardhi. Na Hadiithi pia inabainisha kuwa dalili ya kweli ya Masihi Aliyeahidiwa itakuwa ni kuuvunja msalaba huu na kumuua Dajjal mkubwa. Mamulla au Masheikh wetu wakijinga hawaonekani kuakisi kwamba lengo kuu la Masihi Aliyeahidiwa ni kuvunja msalaba na kuuawa kwa Dajjal mkubwa. Qur'ani Tukufu imebashiri kwamba ule udanganyifu mkubwa na uharibifu ambao kwao utaratibu wa ulimwengu mzima unaweza kufadhaika na kumalizika kwa uovu wa wamishenari wa Kikristo.

Kutokana na hili inafahamika kwa uwazi kwamba hakuna Dajjal mkubwa zaidi kuliko makasisi na kwamba yule ambaye, baada ya kushuhudia kuteremshwa kwa

UK. 04

Mjue Jinni

Kutoka Uk 03..

uovu huu mkubwa, anamgoja mwingine, anakanusha ukweli wa Qur'ani Tukufu.

Zaidi ya hayo, kwa vile maana halisi ya neno Dajjal ni kundi linaloichafua dunia kwa udanganyifu wake, na, kwa mujibu wa Hadith, ishara ya pekee ya Dajjal mkuu itakuwa ni utetezi wake wa msalaba, kama mtu bado atashindwa kuzingatia Makasisi wa Kikristo kama Dajjal mkuu, kwa hakika yeye ni kipofu wa kiroho." (Anjam-e-Atham, Ruhani Khazain, Juzuu 11, Ukurasa 46-48).

DAJJALI NI MTU MMOJA AU TAIFA?

Kwanza, mtu anapaswa kukumbuka kwamba njozi haziwezi kuchukuliwa kiuhalisia.

Zimejaa maana za ndani zaidi na hiyo inaeleweka zaidi tunapokuja kwenye hadithi zinazo zungumza kuhusu Dajjal. Ni kweli kwamba katika Hadith nyingi Dajjal ameelezewa kuwa ni mtu mmoja, lakini tunapozingatia sifa za mtu huyu, inathibitisha zaidi kwamba hii ilionyeshwa kueleza jinsi watu wa taifa hili wangekuwa. Na taifa linaweza kuwakilishwa katika njozi au ndoto kama mtu mmoja tu. Aya za Qur'ani Tukufu za Surah alKahf zinathibitisha zaidi kwamba Dajjal ni taifa na tunapaswa kuzifasiri Hadithi kwa mujibu wa Qur'an badala ya kutafsiri vibaya Qur'an juu ya baadhi ya hadithi ambazo mwanzoni hatuwezi kuzielewa kabisa. Qur'an inamuweka Dajjal katika kundi la mataifa ya Kikristo na inatuonyesha kwamba hakuna tofauti kati yao, na Yajuj na Maajuj. Zaidi ya hayo kwa mujibu wa Qur'an, Ibrahimu a.s mwenyewe anaitwa taifa ingawa tunajua alikuwa mtu mmoja na hakuna anaye pinga hilo. Kwa bahati mbaya wenzetu linapo kuja swala la Dajjali hawataki kufahamu kama taifa wanataka abaki kama mtu mmoja. Tuna soma katika Quran Allah mtukufu anasema katika aya hii kwamba:-

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ حَنِيفًا وَلَمْ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ {121:

Hakika Ibrahim kwa dhati yake alikuwa ni kama taifa zima akiwa mtiifu kwa Allah aliye halisika na wala hakuwa miongoni mwa washirikina. (Sura ya 16 aya ya 121) maana yake ni hii yeye alikuwa na mbegu na uwezo uliyo hifadhiwa wa kuunda taifa kubwa alilo ahidiwa.

Hivyo basi ikiwa Ibrahimu ambaye alikuwa mtu mmoja anaweza kuitwa taifa katika Qur'ani Tukufu, kwa nini dajjal hawezi kuelezewa kama mtu mmoja katika njozi ya Mtume Muhammad s.a.w? Lakini tuki kurejea neno taifa zipo hadithi nyingi zinatuonyesha kwamba Dajjal hakika ni taifa na si mtu mmoja. Mtukufu Mtume saw alisema: ''Mtapigana nao (Waarabu) na Mwenyezi Mungu atakupeni ushindi juu yao; kisha mtapigana na Uajemi na Mwenyezi Mungu atakupeni ushindi juu yao; kisha utapigana na Dajjal na Mwenyezi Mungu atakupeni ushindi juu yao" (Mishkat, baab Al Malahim).

Mtukufu Mtume (s.a.w) ametaja kwa uwazi zaidi vita na Dajjal kwa namna ya vita vingine vya Waarabu, Waajemi na Warumi ambao ni mataifa yote. Hii inaonyesha kuwa Dajjal pia ni taifa na si mtu mmoja kama wengine wanavyo dhani. Maana kuna maneno aliyo tumia kwa kusema juu yao hivyo hapo haimaanishi mtu mmoja bali ni taifa lililo pewa jina Dajjali katika bishara.

Qur'an pia inasema:-

يَا بَنِي إِسْرَائِيلَ اذْكُرُوا نِعْمَتِيَ الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَأَنِّي فَضَّلْتُكُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ {48

Enyi wana wa Israeli! Kumbukeni neema yangu Niliyo wa neemesheni na Nika wapeni fadhilini kuliko viumbe wote." (Sura ya 2 Aya ya 48)

Qur'ani inasema kuhusu Wana wa Israili kana kwamba Mwenyezi Mungu Anazungumza na mtu mmoja. Zaidi ya hayo, Mtukufu Mtume (s.a.w) alituambia tusome aya kumi za mwanzo na kumi za mwisho za Surah al-Kahf, ili tulindwe dhidi ya Dajjal, na zote mbili zinarejea kwenye mataifa. Mtume Mtukufu Muhammad (s.a.w) aliamua kutufanya tuhifadhi aya za kulindwa dhidi ya Dajjal. kama aya hizi hazikuwa na uhusiano wowote na Dajjal Kwa nini alisema tuhifadhi? Ni wazi kwamba aya hizi zinamuelezea Dajjal kwa namna bora kabisa na zimewabainisha kwa uwazi kuwa ni mataifa. Na tafsiri ya ki Ahmadiyya inayo husu Dajjal ndiyo tafsiri pekee inayoendana na Qur-aan na Hadith.

Hazrat Mirza Ghulam Ahmad a.s anasema:- "Dajjal si jina la mtu mmoja Kwa mujibu wa kamusi ya Kiarabu, neno Dajjal linaashiria kundi la watu wanaojionyesha kuwa ni waaminifu na wachamungu, lakini si waaminifu wala si wachamungu.

Bali kila wanachosema kimejaa upotevu na udanganyifu. Tabia hiyo inapatikana katika tabaka la Wakristo wanaojulikana kama makasisi pamoja na mayahudi.

Kundi jingine ni lile la wanafalsafa ambao wanashughulika na kujaribu kuchukua udhibiti wa mashine, viwanda na mpango wa Kimungu wa mambo. Hao ndio Dajjal hasa kwa sababu wanawalaghai viumbe vya Mwenyezi Mungu kwa vitendo vyao na madai marefu kana kwamba wao ni washirika katika ufalme wa Mwenyezi Mungu. Makasisi wanajivuna wenyewe hadhi ya Utume kwa sababu wanaipuuza Injili ya kweli ya mbinguni na kueneza mambo ya potevu na potofu kama tafsiri inayodhaniwa ya Injili." (Kitab-ul-Bariyyah, Ruhani Khazain, Juzuu 13, Ukurasa 243-244). , Tanbihi)

Sababu kubwa inayo fanya katika baadhi ya Hadith Dajjal ajulikanae kama "al-Masih" ni kwa sababu tu Dajjal atakuwa anaeneza uongo kwakutumia jina la Masihi, ambalo alipewa Issa. Jina hili la Masihi, alipewa Issa wa zama zile. Jina hili pia limepewa kwa Dajjal kwa vile litakuwa likifanya kazi mbaya kwa jina la Issa a.s ambayo kwa hakika itakuwa ni uongo mtupu usio na ukweli wowote nyuma yake.

Maana ya Ahadith Zinazoelezea Dajjal

Moja ya Hadith ambazo mara nyingi hunukuliwa kuhusiana na Dajjal ni

حَدَّثَنَا يَحْيَى بْنُ بَكَيْرٍ، حَدَّثَنَا اللَّيْثُ، عَنْ عُقَيْلٍ، عَنِ ابْنِ شِهَابٍ، عَنْ سَالِمٍ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ " بَيْنَا أَنَا نَائِمٌ أَطُوفُ بِالْكَعْبَةِ، فَإِذَا رَجُلٌ آدَمُ سَبْطُ الشَّعَرِ ينظف - أو يُهَرَاقَ - رَأْسُهُ مَاءً قُلْتُ مَنْ هَذَا قَالُوا ابْنُ مَرْيَمَ. ثُمَّ ذَهَبْتُ الْتَفِتُ، فَإِذَا رَجُلٌ جَسِيمٌ أَحْمَرُ جَعْدُ الرَّأْسِ أَعْوَرُ الْعَيْنِ كَأَنَّ عَيْنَهُ عِنَبَةٌ طَافِيَةٌ قَالُوا هَذَا الدَّجَّالُ . أَقْرَبُ النَّاسِ بِهِ شَبَهًا ابْنُ قَطَنٍ رَجُلٌ مِنْ خُزَاعَةَ.".

Imesimuliwa na Hadhrat Abdullah bin Umar r.a kwamba Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w "Nilipolala nilijiona (katika ndoto) nikifanya Tawaf kuzunguka Al-Ka'ba. Tazama, nilimwona mtu wa kahawia mwenye nywele nyororo, na maji yakimtoka kichwani. Nikauliza, "Ni nani huyu?" Wakajibu: Mwana wa Maryamu. Kisha nikageuza uso wangu kumwona mwanaume mwingine mwenye mwili mkubwa, rangi nyekundu na nywele zilizojisokota na kipofu katika jicho moja. Jicho lake lilionekana likichomoza kama zabibu nje. Wakasema (kuniambia), Yeye ni Ad-Dajjal." Mtume (s.a.w) akaongeza, "Mtu anayefanana zaidi naye ni Ibn Qatan, mtu wa kabila la Khuza. "(Sahihi Bukhari, Hadithi namba 7128)

Allah atusaidie kumwelewa vizuri Dajjal na kuweza kujikinga nae sawa na miongozo ya Mtume s.a.w na masihi waka wa zama. Amiin

Itaendelea.... Inshallah toleo lijalo

Wasiyyat

0785 086527-Msaidizi wa Katibu wa Wasiyyat
O750 953918-Naibu Katibu wa Wasiyyat

MASWALI YANAYOHUSU MAPATO:

Maana ya maneno mbalimbali
Hissa: Mchango
Amad: Kipato
Hissa Amad: Mchango ambao Musi anawajibika kulipa sawa na kipato chake halisi, ambao kiwango chake cha chini ni sehemu ya Kumi(1/10) na kinaweza kuongezwa hadi sehemu 1/3.

Hissa Jaidad: Mchango ambao Musi analipa kutokana na mali anayomiliki na analipa baada ya kufanya tathmini rasmi ya Mali yake hiyo.
Jaidad: Mali.
Musi: Mwanaume aliyejiunga na mpango wa Wasia. [mwanamke: Musiah] (wingi: Musian)
Nizam-e-wasiyyat: Nidhamu ya wasia.

Tashkees: Tathmini.
Swali 1: Nidhamu ya Wasiyyat ina michango mingapi muhimu?
Jibu: Miwili nayo ni
(i) Hissa Amad-Mchango sawa na Mapato mfano Mshahara, mapato ya biashara n.k
(ii) Hissa Jaidad- Mchango unaolipwa baada ya kufanya tathmini ya mali inayomilikiwa na Musi.
Zingatia: Ikiwa kama Mali anayomiliki Musi inamuingizia mapato, basi mapato hayo atayalipia Chanda Wasiyyat kwa kiwango cha Chanda Am yaani 1/16

Swali 2: Ni kipi kiwango cha malipo ya Wasia kwenye kipato na kwenye Mali?
Jibu: Musi anatakiwa:
a) Kuweka wasia wa sehemu 1/10 mpaka 1/3 ya mali yake wakati wa kifo chake.
b) Kulipa Chanda Hisa Hissa Amad kwa kiwango cha 1/10 mpaka 1/3 ya kipato chake kutoka vyanzo vyote kipindi cha uhai wake isipokuwa kipato kinachotokana na mali yake.
c) Kulipa Chanda Hissa Amad kwa kiwango cha Chanda Aam (1/16) kwa kipato kinachotokana na mali yoyote.
Swali 3: Wakati wa kujiunga na wasia, kama mtu hana kipato thabiti ataandika nini kama kipato chake cha mwezi?

Jibu: Kama mtu hana kipato thabiti, anaweza kuandika makadirio ya kipato chake kwa wastani wa kipato cha miezi sita au mwaka.

Swali 4: Je kuna muongozo kuhusu wanawake ambao hawana chanzo cha mapato na wanalipa mchango kwa msingi wa fedha ya kujikimu(Pocket Money)?

Jibu: Utaratibu unaotumika Kulipa Chanda wasiyyat kwa mwanamke asiyekuwa na chanzo cha mapato binafsi, ni huu kwamba mume wake anatakiwa kuweka kiwango sahihi kama Fedha ya kujikimu (pocket money) ambayo itatumika kama chanzo cha mapato kwa mwanamke huyo, na yeye kwa madhumuni ya kuendelea kujitolea fedha atalipa Chanda Wasiyyat kutoka kwenye Fedha yake hiyo ya kujikimu(pocket money). Wanawake wanatakiwa kulipa Chanda kulingana na kiwango cha maisha yao.

Kujitolea kunakofanywa na Musi kunatakiwa kuwe kwa kiwango cha juu kuliko kujitolea kwa mtu anayelipa Chanda Aam. Lakini pocket money anayopata haitakiwi kuwa chini ya kiwango kilichowekwa kwa nchi husika anayoishi. (Kwa Tanzania Markaz imeweka kiwango cha chini kwa wale wasio na mapato kuwa Tsh 50,000 kwa mwezi, Ambapo Chanda Wasiyyat atalipa Tsh 5,000/- kila mwezi. Hii sheria haiwahusu wanafunzi)
Swali 5: Je ni lazima kwa Musi mwanafunzi kulipa Chanda Wasiyyat kutoka kwenye Pocket money yake?

Jibu: Skolaship za wanafunzi hazitakuwa na ulazima wa kulipa Chanda katika viwango vilivyowekwa. Bali wanafunzi wanatarajiwa kuwekewa kiwango baada ya kushauriana na jamaat na kulipa ipasavyo.

Swali 6: Pamoja na kulipa Hissa Amad kutoka katika mishahara yao(Full salaries), Mfanyakazi pia huchangia kiasi fulani kila mwezi kwa msingi wa kupokea Pensheni baada ya kustaafu. Je Chanda italipwa kutoka katika Pensheni katika kesi kama hiyo?

Jibu: Ndio, Hissa amad inatakiwa kulipwa kutoka katika Pensheni. Kwa sababu kiasi kinachokatwa kwa mwezi huwa ni kiasi kidogo, Ilhali kiasi cha Pensheni kinachopokelewa wakati wa kustaafu ni kikubwa Zaidi. Ikiwa mtu anataka kukata kiasi hiki katika Pensheni yake, atakata tu kiasi kile alicholipia. Na Chanda italipwa kwenye kiasi kilichobaki.
Swali 7: Ni aina gani ya matumizi yanayotakiwa kuondolewa katika kipato cha mtu kwenye swala la Chanda?

Jibu: Mapato ambayo Chanda inatakiwa kulipwa, yanahusu aina zote za mapato kutoka katika vyanzo vyote. Isipokuwa tu malipo yafuatayo yanaweza kukatwa kutoka katika pato halisi.

(i) Posho wanazopewa wafanyakazi, ambazo matumizi yake hayapo mikononi mwa wafanyakazi.

(ii) Kodi za Lazima zinazotozwa na serikali mfano Kodi, Bima za Lazima, local rates.

(iii) Posho wanazopewa wafanyakazi kwa ajili ya matumizi maalumu mfano Posho za Sare, Posho za Elimu, Posho za Watoto.

(iv) Posho, zinazolipwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya kiofisi mfano Posho za Safari(travelling Allowance (T.A), Per Diem(D.A) hazilipiwa Chanda, lakini endapo kama kuna Kiasi ambacho mtu amekihifadhi baada ya matumizi ya lazima, kiasi hicho anapaswa kulipa Chanda Wasiyyat.
Swali 8: Je kiasi kinacholipwa kwa ajili ya bima ya nyumba (Makazi) kitakatwa kutoka katika Pato halisi kuhusiana na Chanda.

Jibu: Kiasi kinacholipwa kwa ajili ya bima za Nyumba, hata ikiwa ni ya Lazima, hakikatwi kutoka katika mapato yanayohusu Chanda. Ikiwa ni Lazima kuwa na bima ya nyumba ili kukopa kutoka katika Makampuni ya Rehani, Mnunuzi bado ni mnufaika. Hivyo matumizi hayo, yatahesabika kuwa ni ya kawaida. Haitakiwi kukata kiasi chochote cha malipo ya awamu, malipo ya rehani, riba au bima kutoka katika pato halisi la mtu kuhusiana na Chanda.

Swali 9: Je Bima ya Afya inaweza kukatwa kutoka katika pato kuhusiana na chanda?

Jibu: Kiasi kinacholipwa kwa ajili ya Bima ya Afya hakikatwi kutoka katika pato, hata kama ni yalazima. Isipokuwa katika mazingira ambayo inachukuliwa kama ni kodi na faida zake hunufaisha jamii nzima badala ya mtu binafsi au familia.

Swali 10: Ikiwa Musi anamiliki mali isiyohamishika mfano Nyumba, ambayo amepangisha. Je anahitajika kulipa Hissa Amad katika kipato anachopokea kama kodi ya nyumba hiyo?

Jibu: Iwapo kuna mapato yoyote yanayotokana na mali ya Musi basi Hissa Amad italipwa kwa mapato hayo kwa kiwango cha Chanda Aam yaani 1/16.

Bustani ya Washairi

BWANA YULE

Umetufarakanisha, mijini na vijijini
Mwamba ulitujambisha, ulipoketi kitini
Uongo ulidumisha, lipokua ofisini
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Maneno ulitulisha, 'lipokua vikaoni
Kila tulipokumbusha, hukuyaweka kichwani
Kweli Mungu anatisha, umeondoshwa kitini
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Macho ulijipofusha, ulikua hauoni
Kazi uliwafurusha, wasaidizi kundini
Kisa mama kumfusha, hautakiwi kazini
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Hela lijimilikisha, kama zako mfukoni
Kuwapa wanokuosha, wasiokua na soni
Mungu ametuepusha, tutakutana ndotoni
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Ulijawa na Kiburi, haukujali lolote
Maisha ya kifahari, ulipokua popote
Ukweli kwako shubiri, ulitudanganya kote
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Ulijiona jabari, unaamua lolote
Na hukua na muhari, kumfukuza yeyote
Umelipata kaburi, tumezika mambo yote
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Huko Shinyanga hatari, watu lazima wajute
Mambo yake ni shubiri, embu kwanza tema mate
Hukumwogopa Kahari, kwa miaka ile yote
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Watu umewaathiri, ki akili mara zote
Wapo walowasha gari, wanaliza siku zote
Ulijawa na Kiburi, lituumiza sote
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Ulishachomoa panga, kwa wazee na vijana
Kila lile ulopanga, hukupiga dana dana
Na barua za kutunga, ulizitoa mchana
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Uongo uliutunga, kutwa kusimamishana
Ulizidi kubananga, kutofokea mchana
Hotuba zisizojenga, zimewaua vijana
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Misikiti ulijenga, ulifanya la maana
Wafuasi wa kutunga, wala hawakukutana
Kweli Mungu sio Bunga, mitandao 'mekuchana
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Walimu mwenye majanga, walidhalilika sana
Ulisema wanatunga, wajaribu kujibana
Wewe ni mchuma janga, utapata tabu sana
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Kwa kweli tulidhikika, Mungu wetu 'mesikia
Bwana amekamatika, kutwa kucha analia
Eti tutamkumbuka? Watu watajililia
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Ulijidai mtata, familia zimelia
Matibabu ulikata, walimu wakajifia
Sisi lazima kujuta, kwa uliyotufanyia
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Na muda haukupata, watu kuwatembelea
Imani zilizorota, michango ikapotea
Kwa kweli tulikopita, machozi yalikolea
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Mimi hapa sitajuta, kwa uliyo tufanyia
Kwa kweli ulitusuta, kila ukihutubia
Wasalimie Kapurta, zamu yao kupitia
Sitajutia chochote, nenda usirudi tena.

Abdallah Kalindima
#Chuma Chakavu (kalindimasenior@gmail.

KARIBU AMIRI WETU

Mungu ametukumbusha, kwa uwazi na mapema
Sala tulibidiisha, twakushukuru Karima
Karibu Kiumbe tosha, tumesuuzwa mitima,
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Umejawa na bashasha, na uso wenye huruma
Hauigizi maisha, hupendi kusema sema
Mola anatukumbusha, Wamakonde Wamanyema
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Vinyongo tumevishusha, tumeshaacha kuhema
Kwangu Mimi naonyesha, nimefanya takirima
Makundi sambaratisha, watu wote tuwe wema
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Nyuso zetu tumeosha, zimejawa na hekima
Upendo wako watosha, metuonesha mapema
Ukiwa pale Arusha, waumini wamesema
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Ewe Sheikh unatosha, kuunganisha uma
Najua hutapotosha, kila kitu utasema
Tunasema unatosha, hutaturudisha nyuma
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Kiumbe mwenye bashasha, hutaumiza mitima
Sisi tutajidogosha, tunakwambia mapema
Wahaya na kina ngosha, nawakumbusha mapema
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Mola atatuepusha, Kila kukicha kusema
Kila uchwao kushusha, lawama kama Mlima
Ndugu nina wakumbusha, tuache kusema sema
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Myoyo utaiamsha, ile yote ilo zima
Kundini kuwarudisha, walozama kwa kisima
Na wale walotingisha, wasimame kutusema
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Sala utatusalisha, na hotuba utasoma
Wala hutatugombesha, kwa sauti yenye wema
Upendo utadumisha, bila kutusema sema
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Umeshatufarijisha, ulipokua Dodoma
Nyumbani ulitulisha, bila kusahau nyama
Ulikua na bashasha, kwa watu wenye zahama
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Choyo haujatuonyesha, ni kiongozi wa uma
Tumeshakukaribisha, wewe pamoja na Mama
Tuko tayari kukesha, kuilinda hii zama
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Tukija hodi kubisha, uendeleze huruma
Na wali wakushibisha, atupakulie Mama
Nyama ziwe za kutosha, wengine ni Wasukuma
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Hotuba kutushibisha, kwa maneno ya huruma
Maovu kuainisha, huku tumeshika tama
Dini inatukumbusha, sio mbele sio nyuma
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Na hatutajitunisha, pale utapotusema
Vichwa tutainamisha, kusikiza 'nachosema
Ndimu tutaigubisha, na mate hatutatema
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Na wala hatutazusha, pale tutakaposema
Nyonyo zitatukumbusha, uungwana ndio dhima
Mada hatutarefusha, hakitakua kiama
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Moyo wa aina gani, kila nikiukumbuka
Uso umejawa soni, kusema ya uhakika
Wewe ni kabila gani, hujapata kulimbuka?
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Unapita majumbani, unasalimia rika
Huna Roho ya kwanini, wala hauna mahoka
Ukiwa madhabahuni, machozi yanakutoka
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Tuishio mtaani, tunaishi kwa kucheka
Makasiriko ya nini, si viumbe wa Rubuka
Haya maisha ni nini, kuishi bila vibweka?
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Magari ya kazi gani, gereji kuyarundika
Mahubiri kwani lini, mji tutauzunguka
Huna Sumu kwenye ini, ndo mana huna vibweka
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Tutasogea kundini, hilo nina uhakika
Waloingia mitini, wote watabadilika
Kiongozi una dini, na mengine kadhalika
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Tukianza mikoani, machozi yabubujika
Upendo 'mekua duni, pembeni wamejiweka
Uanzie tangu chini, kuunga palokatika
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Sisi sote waumini, dini tumeshaishika
Ila hali zetu duni, wengi wetu tumechoka
Utupe konekisheni, Mungu atakukumbuka
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Hali za wazazi duni, na mengine kadhalika
Wajapo msikitini, nyuso zao 'medhikika
Elimu ya juu duni, upate kuwakumbuka
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Ewe ndugu muumini, jipange kubadilika
Jitoe huko mwituni, kiongozi amefika
Iwe ulifanywa nini, jirudishe Mwanameka
Mapenzi yalotukuka, karibu ukaribie.

Sisi sote wa kundini, ujinga tumekomboka
Hatutasema wa nini, kama vikieleweka
Sisi ni wa Jamatini, si rahisi kugeuka
Nakukaribusha tena, Amiri wa zama hizi

Abdallah S. Kalindima
#CHUMA CHAKAVU
kalindimasenior@gmail.com
26 June, 2024
23:45pm

Wanawake makazini

Wanawake mnanini, viti mnapokalia
Mwawa wakali kwanini, kufoka mumezoea
Mewalazimisha nani, nafasi mliyokaa
Nenda kakaenyumbani, kama kazi yakuboa

Kisirani we kwanini, mteja kihudumia
Naumbea we wanini, wateja kupuuzia
Umnyonge nikwanini, kazi ulojitakia
Nenda kakaenyumbani, kama kazi yakuboa

Masihi omary stambuli.Kisagwa

Hadithi ya Hamasa ya Kiislamu:

Kujaribu Pancake

Mvulana mwenye umri wa miaka sita aliamua asubuhi moja kuwatengenezea wazazi wake chapati.

Alipata bakuli kubwa na kijiko; Akavuta kiti kaunta, akafungua kabati



na kuchomoa kopo la unga mzito na kumwaga chini. Alichota unga ndani ya bakuli kwa mikono yake, akachanganya katika kikombe cha maziwa na kuongeza sukari, akiacha njia ya unga kwenye sakafu ambayo kwa sasa ilikuwa na nyimbo chache zilizoachwa na paka wake. Alikuwa amefunikwa na unga na kupata kuchanganyikiwa.

Alitaka hili liwe jambo jema sana kwa wazazi wake, lakini lilikuwa linazidi kuwa mbaya. Hakujua la kufanya baadaye, ikiwa ni kuweka yote kwenye oveni au kwenye jiko, (na hakujua jinsi jiko linavyofanya kazi!).


Ghafla aliona Paka wake akilamba kutoka kwenye bakuli la mchanganyiko na kufikia kumsukuma mbali, akipiga katoni ya yai chini. Kwa hasira alijaribu kusafisha uchafu wote lakini akateleza kwenye Mayai, na nguo zake za kulalia zikiwa nyeupe na kunata.

Na hapo hapo akamuona Baba amesimama mlangoni.

Machozi makubwa yaliwatoka. Alichofanya alitaka kufanya kitu kizuri, lakini alifanya fujo mbaya. Alikuwa na uhakika kuwa karipio linakuja, labda hata kuchapwa. Lakini Baba yake alimtazama tu. Kisha, akitembea kwenye sakafu, akamchukua mtoto wake aliyekuwa analia, akamkumbatia.

Maadili ya Hadithi:
Hivyo ndivyo Allah anavyoshughulika nasi. Tunajaribu kufanya kitu kizuri maishani, lakini kinageuka kuwa fujo. Ndoa yetu inanata au tunamtukana rafiki au hatuwezi kustahimili kazi yetu au afya yetu inadhoofika.
Wakati mwingine sisi husimama pale tu kwa machozi kwa sababu hatuwezi kufikiria kitu kingine chochote cha kufanya. Hapo ndipo Allah anapotuchukua na kutupenda na kutusamehe. Lakini kwa sababu tu tunaweza kuvuruga, hatuwezi kuacha kujaribu «kutengeneza pancakes» Mapema au baadaye tutairekebisha, na kisha watafurahi kuona kwamba sisi angalau tulijaribu...
Nukuu ya Kuhamasisha:
«Mafanikio sio ya kudumu na kutofaulu sio mwisho. Kwa hivyo, usiache kufanya kazi baada ya mafanikio na usiache kujaribu baada ya kushindwa."

Unganisha Nukta kupata Mchoro



JINSI YA KUPIKA KARANGA ZA MAYAI

MAHITAJI

✓ Karanga kilo moja.
✓ Mayai 3
✓ Chumvi kijiko kimoja.
✓ Sukari kiasi unachohitaji.
✓ Unga wa ngano robo kilo(kidogo tu).
✓ Mafuta ya kupikia.

JINSI YA KUANDAA

✓ Chukua karanga weka katika sinia, chambua kuondoa karanga mbovu, zilizokatika na taka taka.
✓ Baada ya kuchambua weka katika bakuli au chombo cha kukandia, piga mayai katika chombo pembeni na uweke chumvi.
✓ Tia mayai katika karanga na kisha zichanganye kuhakikisha zote zimekolea mayai.
✓ Chukua kiasi cha sukari unachokadiria kitakufaa Tia katika ule mchanganyiko wa karanga, mayai na chumvi kisha Changanya ili sukari inate katika karanga zote.
✓ Chukua unga Tia Katika mchanganyiko wako, changanya vizuri kuhakikisha karanga zote zimekuwa nyeupe kwakufunikwa na unga.
✓ Weka mafuta kiasi kwenye kikaango, yakichemka anza kukaanga karanga zako hakikisha unazitoa kabla hazijawa Brown sana usijeunguza karanga zako.





✓ NB: KAMA UNAPIKA ZA BIASHARA UKISHAZIEPUA KUWA MAKINI NA WATOTO KWA SABABU WANAPENDA KUZIDOKOA HATARI HAUKAWII KUKUTA ZIMEISHA. TAMU:

✓ HIi ni Biashara Mzuri Sana Wanafunzi wangu, Unaweza kutafuta Watu ambao unawaamini ili wakusambazie na kukuuzia kwenye Mikusanyiko ya Watu au Unaweza Kuifanya hata Nyumbani kwako.

Maisha baada ya kifo

ya wanamazingahombwe na hutawaliwa na namna tofauti za sheria kabisa. (Q.17:v.14 - 15) Kwa kifupi, ulimwengu wa ndoto na Kashf hutumika kama kielelezo cha maisha yajayo na kumwezesha mwanadamu kutambua asili ya maisha ya ulimwengu ujao. Kama vile vitu vyote katika ndoto ni vya kiroho, na bado vina mwili, vivyo hivyo vitu vya maisha yajayo vitakuwa na mwili, lakini mwili huo utakuwa wa kiroho na sio wa mwili, na roho itafanya kazi za kiroho bado juu zaidi katika kiwango.

Qur'ani Tukufu inaeleza hali za maisha yajayo hivi: Inasema kwamba matendo yanayofanywa na mwanadamu katika maisha haya yatachukua umbo katika yajayo. Kile tunachoita maji ya ulimwengu ujao kitakuwa kielelezo cha matendo ya mwanadamu aliyoyafanya kulingana na sheria ya Mungu. Maziwa ya maisha yajayo yatakuwa ni Elimu ya Mungu ambayo mwanadamu anapata katika maisha ya sasa. Matunda ya mbinguni yatakuwa kielelezo cha radhi na furaha ambayo roho ya mwanadamu inahisi katika kufanya utii kwa Mungu.

Quran Tukufu inasema: 'Matendo ya mwanadamu yanabaki kushikamana naye na kamwe hayatenganishwi naye. Athari zao zimefichika, lakini Siku ya Kiyama tutazigeuza kuwa kitabu atakachokisoma, yaani athari zao zitadhihirika na kila amali aliyoifanya mwanadamu katika maisha haya itazaa matunda yake na kuyatengeneza maisha ya ulimwengu ujao kulingana na asili yake, 'Tutamwambia mwanadamu, 'Sasa endelea kusoma kitabu hiki,' yaani, endelea au kurudi nyuma kulingana na tabia ya matendo yako na uvune matunda yake. 'Hatuna haja ya kuhesabu matendo yako. Nafsi yako itaendelea kuhesabu matendo yako, yaani, athari ambazo amali zako zimeleta zinakutosha kuwa ni malipo na adhabu. Hatuna haja ya kukuadhibu yoyote mpya au kukupa malipo mapya. (Q.17:v.14-15.)

Tazama jinsi aya inavyosema kwa uwazi kwamba thawabu na adhabu za ulimwengu ujao ni mifano ya matendo ya mwanadamu katika maisha haya. Mahali pengine Quran Tukufu inasema: 'Watu wema watakunywa kikombe, ambacho kitakuwa na mchanganyiko kafuri,' yaani, kitakuwa na fadhila ya kukandamiza tamaa mbaya. 'Vikombe vitajazwa katika chemchem ambayo Waumini wameichimba kwa kazi kubwa,' yaani, matendo waliyoyafanya Waumini katika maisha yao ya duniani yangetokea katika ulimwengu ujao kwa namna ya chemchem (Q.76: v.6-7) Tena, Quran Tukufu inasema;. , 'Aliye kipofu katika dunia hii atakuwa kipofu katika siku zijazo.' (Q.17:v.73) 'Yaani mtu ambaye hajauona ukweli kwa jicho la nafsi yake katika ulimwengu huu atahisi kana kwamba alikuwa kipofu katika wakati ujao, kwani nafsi ya maisha haya itakuwa mwili wa yajayo.

Katika sehemu nyingine, Quran Tukufu inasema: Na yule asiyejali kunikumbuka katika maisha haya na hajali kunitafuta ataishi maisha ambayo yataendelea kupunguza nguvu zake za kiroho na matokeo yake yatakuwa mabaya. Wakati ambapo nafsi inapaswa kuwa imekamilisha nguvu zake na kuzaliwa katika hatua inayofuata ya kiroho, mtu kama huyo angekuwa kipofu, (yaani, angezaliwa kipofu katika maisha yajayo). Kisha katika hali ya mshangao husema: Ewe Mola wangu Mlezi! vipi haya yote yametokea? Nilikuwa na macho katika maisha yangu ya awali. Kwa nini umeniumba kipofu sasa? Hapo Mungu atasema, "Wewe vivyo hivyo umeliacha neno langu; Mimi sasa nimekuacha upate hatima yako, ili ulipwe kwa kadiri ya matendo yako." (Q.20:v.125-127)

Hii inaonyesha kuwa upofu katika maisha yajayo utatokana na upofu wa kiroho katika maisha haya. Kwa hivyo ni wazi kwamba ingawa thawabu na adhabu za ulimwengu ujao zitakuwa na aina fulani ya mwili, lakini zingekuwa mifano tu ya matendo ya maisha haya, na si kitu kipya kabisa. Maelezo, kama yalivyotolewa katika Quran Tukufu, ya maisha ya ulimwengu ujao pia yanaunga mkono hitimisho hili. Kwa mfano, Quran Tukufu inasema, kwamba watu wa Peponi watanyweshwa mvinyo ambayo itazitakasa nafsi zao. Ni wazi kwamba kitu cha kimwili hakiwezi kuitakasa nafsi.

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

MATUKIO KATIKA PICHA

Jalsa Salana UK Yatikisa

Muhammad[saw].

Watu kutoka pande zote za dunia, wakiwemo waahmadiyya na wasiokuwa waahmadiyya walimiminika katika viwanja vya Hadiqatul Mahadi ili kuhudhuria mkutano ambao Masih Aliyeahidiwa[as] alisema kuwa si sawa na mikutano hii ya kidunia. Vijana kutoka katika Jamati nyingi walikuja maalum kushiriki katika kuwatumikia wageni wa Masih Aliyeahidiwa[as] kuwapokea wageni hao wenye tamaduni tofauti, kuwahudumia kwa tabasamu, upole na hekima ni Muujiza unaweza kuelezwa tu na neno *Msaada wa Allah*. Chakula, maonesho, malazi, ulinzi, matangazo yote hayo yanafanyika katika siku tatu ambazo zinaambatana na hotuba za wataalamu wa Jamati na bilhususi hotuba za Kiongozi wetu mpendwa Khalifatul Masih wa V Hazrat Mirza Masroor Ahmad[atba].

Katika toleo letu lijalo tutawaeleza in shaa Allah yaliyojiri katika mkutano huo uliomalizika tarehe 28-07-2024.

Masjid Salaam wakifuatilia Jalsa Salana pamoja nae Amir Sahib Tanzania. Sambamba na Kitonga pamoja nae Ustadh Issa Malenge Sahib



ANGUKO LA MTU LIPO KWENYE KILELE CHA MAFANIKIO YAKE

Na.
Maulana Sheikh Shahab Ahmad



Kwa muda mrefu sasa nimekuwa nikishuhudia ya kwamba watu wengi ambao walinyanyuka katika mafanikio na umaarufu mara walikufa ghafla iwe kwa ajali au vifo ambavyo wengi wa mashabiki zao tuliishia kushangaa na kupatwa na woga.
Kwa upande mwingine baadhi ambao walifikia katika madaraja hayo waliishia katika ajali kali ambazo wengi zilitufanya kufikiria tena msemo wa kiswalihili usemao, “Ngoma ikivuma sana hupasuka”
Mara nyingi mwisho wa mwaka unakuwa hatari mno, kwani ajali nyingi za barabarani hutokea lakini pia misiba huwa mingi mno, binafsi Baba yangu mzazi alifariki mwisho wa mwaka uliopita mwezi wa kumi na mbili na vivyo hivyo wakati siku ya christimas 2023 wenzangu wakisherehekea mimi nilikuwa safarini kwenda kumzika Bibi yangu mzaa Mama ambaye alitulea baada ya kufariki Mama yetu mzazi, lakini cha kushangaza sasa nilipokuwa kwenye gari wengi wasafiri kati yetu walikuwa wanaenda msibani, nililigundua hilo kutokana na simu ambazo walikuwa wakipigiwa na kupiga.
Hivyo ni kusema kwamba kilele cha mwaka nacho huvutia mno ajali na vifo vya watu.
Kwa sababu Mimi ni mtu wa Tanga na kijana mfano mzuri wa ninachotaka kukieleza ni kifo cha kijana wa umri wetu Hussein Ramadhani ‘Sharo Milionea’ ambaye alifariki katika ajali ya gari akielekea kuwaona wazazi wake nyumbani Muheza.
Cha muhimu na kunukuliwa ni kwamba wakati ule ndio alikuwa katika kilele cha umaarufu wake katika uigizaji na hata katika muziki, moyo wangu uliumia sana kwa kuzima kwa kijana ambaye alikuwa anachangamsha maisha ya vijana.
Lakini kiwanda cha Muziki mwaka 2023 kiliona muamko mkubwa wa Muziki wa Amapiano, Mziki ambao asili yake ni Afrika kusini ukiandaliwa mara ya kwanza na Dj Maphoria na Kabza de small, inabidi nieleze jambo hili ili maelezo yangu yalete maana.
Kwenye makala ya mahojiano alieleza kwamba Muziki huu alikuwa anaupiga biti zake katika maonyesho mbali mbali, siku moja aliupiga katika uwepo wa mwanamuziki mkubwa Afrika Wizkid naye akasema huu muziki mbona kama unavutia, ndipo Dj Maphorisa aliingia studio na kuanza kuupunguza ukali wake kwani ulikuwa unasikika vibaya mno, yaani ngoma zilikuwa juu mno, baada ya hapa alianza kuwashirikisha vijana wengi waimbe huu muziki na alikusanya vijana wengi na kuwatengenezea Albam kupitia aina hii ya muziki.
Ndipo walipotoa muziki huo na ulikuwa unasikika kila sehemu hakuna mtu ambaye angeweza kuuzima tena wala kuukataa kwani ulikuwa kila sehemu na vijana wengi wameingia humo, huku unasikia Izolo, huku Adewele huku Focalistic yupo kila sehemu.
Lakini misiba iliyoikumba amapiano ni ya kutisha mno, Mpura na Killer Kau walifariki katika ajali mbaya ya gari kiasi kwamba hakuna wa kusimulia kilichotokea, walifariki watu sita katika ajali ile iliyotokea Augost 2021 na wa saba aliyenusurika alikuwa
amelala pindi ajali ilipotokea na alizinduka hospitalini akiwa anasikia wale aliokuwa nao kuwa wanasemwa ‘walikuwa’ watu wazuri.
Lakini wote hatuwezi kusahau kifo cha jukwaani cha msanii Costa Titch wa maudhui hayo hayo kijana ambaye alikuwa ndio amesaidiwa na lebo ya Akon na kutoa remix ya wimbo wake Big Flexa na alianguka jukwaani na kufariki katika tamasha ambalo mwenyewe alikuwa anatamani siku moja aje kutumbuiza.
Cha muhimu ninachotaka kukieleza ni kwamba binadamu anapofikia kilele fulani basi huanza kuanguka lakini pia kama sivyo anaweza kufariki. Lakini wapo ambao wameendelea na kasi yao nzuri na kuendelea kung’ara katika Nyanja zao na wapo ambao wamefaidi matunda ya wanachokifanya mpaka walipotutoka tuliishia kushukuru na kusema mwacheni akapumzike na akale matunda ya mema aliyoifanyia dunia na ulimwengu. Mwingine tumesema ni upepo tu ukivuma upande wako utaonekana na ukipita atainuka mwingine, lakini Je hakuna yeyote ambaye ameweza kuhifadhi baraka hizi kwa mda mrefu?
Hapa ipo siri nami siri hiyo nimejaribu kuitafakari na kujaribu kuileta ili tuitafakari kwa pamoja. Msanii wa filamu Jamie Foxx wa nchini marekani aliulizwa kuhusu kwanini mtu anapochukua tuzo kubwa kama Oscar anashindwa kurudi tena au anapotea kabisa?
Katika majibu yake alisema huo ndio ukweli hivyo basi mtu anapojiona anapanda katika wadhifa au kazi fulani basi ni lazima apate muda wa kupumzika ili kutengeneza mipango na mikakati ya kurudi upya.
Bahati mbaya iliyomkuta Will Smith ambaye alimzaba kibao Chris Rock kwenye usiku wa tuzo ya Oscar, kwa sababu ya kumsema mwanamke ambaye alimuita mkewe kumbe hawana hata mahusiano ya urafiki kwani ndoa ilishavunjika na baada ya tukio lile sio maanguko tu bali hata yeye mwenyewe ameonekana akiwa dhaifu siku baada ya siku. Alifikia kilele na kuanguka ghafla kama mtu aangukavyo kutoka juu ya mnazi kwani hakuna tawi la kupunguza kasi ya kuanguka. Katika hotuba yake ya shukurani katika usiku huo wa tuzo huku akilia alisema mda mchache uliopita kuwa Danzel ameniambia “Wakati wako wa juu kuwa makini, hapo ndipo shetani anakuja kwa ajili yako”
Tukiangalia kwa undani ni kwamba Mwenyezi Mungu anakinyanyua chochote ili kuleta faida katika ulimwengu au jamii, pale ambapo kitu hicho au binadamu huyo anapoanza kuenda kinyume na jukumu la kuinuliwa kwake basi hufutwa au hupewa onyo au kile alichopewa kama hakitumii vizuri huondolewa.
Je, mlidhani ya kwamba Tumewaumbeni bure na ya kwamba ninyi Kwetu hamtarudishwa? (23:116)
Hivyo kila kitu na kila kiumbe au kila jambo linalotokea ni lazima linadhumuni lake ndani yake, na hivyo chochote kile kikifeli kutimiza majukumu yake na kwenda kinyume basi ni kazi ya Allah kukikumbusha au kukipokonya au kukiondoa.
Nilitaka nielezee kwanza wale ambao huwaka na kuvuma kwa muda kisha baada ya muda anapotea au kuzimika. Kwa upande wangu huwa nachukulia jambo lolote linalovuma katika dunia iwe ni katika mitandao au matukio yoyote katika jamii yetu ni kwa ajili ya kunisaidia kupita katika kipindi fulani ambapo nikiwa natumikia lengo langu fulani. Ndio maana huwa sikubali kubebwa na wimbi la kisiasa wala ubishi wa mpira wala nyimbo za wasanii kwani nimejiwekea kuwa zitapita mimi nitabaki na nitaulizwa juu ya majukumu yangu na hivyo vyote Allah huvituma kwa ajili ya kunifunza na kunichangamsha kuelekea lengo kuu. Ama basi wale ambao huinuka na kuzima jibu lao lipo katika hadithi hii ifuatayo:
Imesimuliwa na Hadhrat Anas (ra) kwamba ngamia jike wa Mjumbe wa Allah aliitwa jina la adhbaa ambaye (alitembea haraka hata) ngamia mwingine yeyote alikuwa hawezi kumpita wala hata kumkaribia kumpita katika mwendo, lakini safari moja akaja bedui mmoja juu ya ngamia wake na ngamia huyo akampita ngamia wa Mtume[saw].
Waislamu wakahuzunika kwa habari hiyo hadi Mtume[saw] akapata habari na akasema: Ni desturi ya Allah ya kwamba kitu kinaponyanyuka juu katika dunia yeye hukishusha chini (ili kisiwahi kujivuna) (Bukhari)
Mara nyingi mtu anapotaka kutoka humshirikisha Mungu kwa nguvu zote na anapofanikiwa huyanasibisha mafanikio hayo na nguvu na uwezo wake wa kutengeneza mitego na mbinu, hayo yote yanamfanya ajione na kujitukuza na kujiona chochote kitu, hapo ndipo Allah humpoteza au humzima kwa mapigo mbali mbali.
Kipindi kile waislamu walipohamia Ethiopia walimsadia Najash katika vita na maswala mbali mbali, inasimuliwa kuwa katika vita fulani ambapo Najash alishinda vita hiyo, katika kusherehekea yeye alikaa chini ambavyo ni kinyume na hadhi ya kifalme, lakini Najash aliwaambia kuwa ukikaa chini basi Mwenyezi Mungu anakunyanyua.
Unyenyekevu ni jambo muhimu sana katika mafanikio ya mtu na mtu kuzidi kunyanyuka katika maisha, na hayo yameelezwa katika hadithi nyingi za Mtume[saw].

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Maisha baada ya kifo

Kutoka 12..

baada ya kifo kukanyaga njia ambayo imetengeneza kutokana na matendo yake. Hadithi iliyonukuliwa hapo juu inatumia neno 'kaburi.' Hata hivyo, haimaanishi kaburi lililochimbwa katika ardhi ambamo mwili umewekwa, bali inaashiria mahali ambapo roho hukaa baada ya kifo. Quran Tukufu inasema, 'Mwenyezi Mungu humfanya kila mtu afe na humtia kaburini.' Ni dhahiri, hata hivyo, kwamba kila mtu hawekwi kaburini; wengine huchomwa moto, wengine huliwa na wanyama wakali na bado wengine hupata mahali pa kupumzika baharini. Kaburi linaashiria kaburi ambalo roho inakaa, na sio mahali ambapo mwili usio na uhai unatupwa, hapo ili kubaki na kutimiza sheria ya milele ya kuoza.

Asili ya Thawabu na Adhabu za Maisha Baada ya Kifo

Asili ya thawabu na adhabu za maisha ya baada ya kifo nitajaribu tena kueleza kama thawabu na adhabu za maisha baada ya kifo ni za kimwili au za kiroho. Uislamu unafundisha kwamba ni za namna zote mbili, ni za kimwili kwa maana ya kwamba nafsi itakuwa imekuza mwili mpya katika maisha yajayo, na uchungu na raha za maisha hayo zitaweza kuhisiwa na kushuhudiwa na mwili huo kama vile mambo ya ulimwengu huu yanavyohisiwa na uzoefu na hisia zetu za kimwili. Zitakuwa za kiroho kwa maana hii kwamba, hazitashiriki asili ya kimwili ya vitu vya ulimwengu huu, kwa maana lengo la kutafsiri nafsi kutoka katika ulimwengu huu hadi mwingine mba inapaswa kuwezeshwa kupata mawazo hayo bora kwa njia ambayo inaweza kutambua dhana hizo nyeti, ambazo mwili wetu huu mzito hauwezi kuwa na uzoefu. Kwa hiyo, inajuzu kwamba mambo ya ulimwengu ujao lazima yawe ya asili tofauti na yale tuliyoyazoea katika ulimwengu huu. Iwapo tutalishwa katika ulimwengu ujao kwa maziwa na asali na matunda kama haya, na moto na moshi wa ulimwengu ujao hautatofautiana na moto na moshi wa dunia hii, basi kusingekuwa na maana katika kuleta utengano wa roho na mwili. Katika hali hiyo tungepaswa kuruhusiwa kubeba miili yetu ya kimwili pamoja nasi. Tumeona kwamba miili ambayo tutawekezwa nayo katika ulimwengu ujao, itakuwa ya asili ya roho zetu katika ulimwengu huu. Je, itawezekanaje basi kwamba chakula cha miili hiyo kiwe maziwa na asali ya dunia hii, na maumivu na adhabu zake ziwe za asili ya moto na maji yanayochemka ya dunia hii? Je, nafsi tulizo nazo sasa zinaweza kutumia moto na maji na matunda ya dunia hii, ili ziweze kuzitumia katika siku zijazo? Kwa hiyo, si sahihi kusema kwamba mwanadamu angepatwa na maumivu au raha baada ya kifo, vyenye asili ya maumivu ya kimwili na raha za dunia hii. Kwa upande mwingine, mambo ya ulimwengu ujao, ingawa si ya kimwili, yatakuwa miili dhaifu ya kiroho na kuonekana kama mtu mbele ya mwanadamu— mambo maovu kwa watu waovu na mema kwa wema. Fahamu na mtazamo wa maisha hauwezi kuwa mkamilifu mpaka vitu dhaifu zaidi viwekewe na mwili dhaifu unaolingana. Kila nafsi inahitaji mwili, mtu mbovu anahitaji mwili mbovu na mzuri anahitaji mwili mzuri. Kwa vile kila nafsi itawekewa mwili katika ulimwengu ujao, mambo ya ulimwengu huo yataonekana kwa hisia za nje za mwili huo kwa namna ile ile ambayo mambo ya ulimwengu huu yanaonekana kwa hisia zetu za kimwili hapa. Lakini jinsi mwili huo utakavyokuwa wa asili ya roho, vitu vilivyofanywa kuwa mtu vya ulimwengu ujao pia vitakuwa vya kiroho. Kama vile katika ulimwengu huu kuna hali za kiroho pamoja na hali za kimwili, hivyo kwa nafsi mpya iliyoumbwa na iliyoinuliwa zaidi ya ulimwengu ujao, kutakuwa na hali za kiroho ambazo zitakuwa bora zaidi kuliko hali ya kiroho ya ulimwengu huu; na kama katika maisha haya, raha na maumivu ni ya kimwili na ya kiroho, hivyo katika maisha yajayo thawabu na adhabu hazitakuwa za kimwili tu bali pia za kiroho. Lakini hali za maisha yajayo zitakuwa za kiwango cha juu zaidi kuliko hali ya maisha haya, kiasi kwamba hali ya mwili ya maisha yajayo italingana na hali ya kiroho ya maisha haya, na hali ya kiroho ya maisha yajayo zitakuwa juu zaidi. Hakika Qur'an Tukufu inazungumza juu ya moto, baridi, hifadhi, nk, kama vitu ambavyo mwanadamu angeadhibiwa navyo katika maisha yajayo, na vivuli, mito ya maji, maziwa na asali kama malipo ya maisha yajayo, lakini wakati huo huo inasema:

Nafsi yo yote haijui waliyofichiwa katika kinachofurahisha macho; ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyafanya. (Q.32:v.18).

Akizungumzia baraka za maisha yajayo, Mtukufu Mtume[saw] anasema, 'Hakuna jicho lililoziona, wala sikio halijasikia, wala akili ya mwanadamu haiwezi kuunda dhana yoyote juu yake.' Sasa ikiwa baraka za maisha yajayo zinapaswa kuwa aina zilezile za karama za Mungu ambazo tunafurahia katika maisha haya, tunapaswa kuwa na uwezo wa kuunda wazo lao, haijalishi ni bora jinsi gani. Lakini maneno ya Mtukufu Mtume (sa) yanaonyesha kwamba baraka za maisha yajayo zitakuwa tofauti kabisa na baraka za maisha haya. Ndivyo itakavyokuwa kwa uchungu na adhabu za maisha yajayo. Quran Tukufu inasema yatakapowekwa matunda ya mbinguni mbele ya watu wa Peponi watasema: 'Haya ndiyo tuliyo ruzukiwa kabla' (Q.2:v.26). Tena kwa kurejelea usemi wao huu Qurani Tukufu inasema, 'Watapewa mfano wake.' (Q.2:v.26). Ndiyo kusema, vitu hivyo havitakuwa vya dunia, bali vitafanana na mambo ya dunia hii katika mwonekano wao wa nje. Ukweli mba ingawa roho haitumii vitu vya kimwili kama mwili unavyofanya, lakini inashiriki katika starehe na maumivu ambayo mwili hupata. Kwa hiyo, kwa vile nafsi imezoea mambo ya maisha haya, ndivyo, ili kukamilisha kipimo cha raha au maumivu yake, mambo ya maisha yajayo yatafanywa kuchukua umbo la mambo ya maisha haya.

Ili kutuwezesha kutambua kwa kiwango fulani hali ya kiroho ya maisha yajayo, Qur'an Tukufu inataja kielelezo cha kutusaidia katika utambuzi huu.

Inasema:

Mwenyezi Mungu Huzichukua roho za viumbe wakati wa kifo chao; na zile zisizokufa, katika usingizi wao. Basi Huzizuia zile Alizozikidhia mauti na Huzirudisha nyingine mpaka wakati uliowekwa. Bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa watu wanaotafakari. (Q.39:v.43).

Hiyo ndio kusema, muunganisho wa roho hutenganishwa kwa muda na mwili hata katika usingizi na hali za maisha baada ya kifo zinaweza kuonekana kwenye mlinganisho huu. Kwa vile utengano huu ni wa muda, roho huhifadhi uhusiano wake na ubongo, ambapo mwanadamu huwezeshwa kukumbuka kile ambacho roho imepitia wakati wa kujitenga kwake na mwili. Qur'ani Tukufu inasema: 'Hapa zipo ishara kwa wanaofikiri,' yaani, mwanadamu anaweza kupata manufaa mengi kutokana na uchunguzi wa hali hii, kwani, anaweza kuelewa asili na matendo ya nafsi na hali yake baada ya kufa. Katika usingizi, mwili unapumzika kwa raha kitandani, lakini mwanadamu hujiona katika sura zingine na kutembelea sehemu mbalimbali. Vitu anavyoviona katika ndoto zake vina miili kama miili ya vitu vya kimwili, wakati mwingine kamilifu sana hivi kwamba vinaacha nyuma ushahidi wa asili yao ya kimwili kwenye mwili wa mwanadamu, jambo linalojulikana sana kwa wale ambao wana uzoefu wa mambo kama hayo. Mimi mwenyewe nimepata uzoefu huu mara nyingi. Wakati fulani, nilikuwa nimefunga saumu na nikaanza kuhisi kiu sana. Kiu yangu ilipozidi na kufikia kutovumilika, nilimwomba Mungu, na kutokana na maombi hayo, niliingia katika hali ya usingizi mwepesi wakati huo kitu kiliwekwa kinywani mwangu ambacho kilikuwa na athari ya kutuliza kiu yangu. Hali hii ilidumu kwa sekunde moja tu, lakini nilijikuta sina kiu tena na nilijiona kama vile nimekunywa maji na kutosheka. Masihi Aliyeahidiwa (as) pia ameandika matukio mengi kama hayo yake mwenyewe. Wakati mmoja, katika hali ya kuwa macho kabisa alimwona Yesu wa Nazareti (as) katika mwili wake wa kiroho, na kufanya mazungumzo marefu naye kuhusu uharibifu ambao ulikuwa umeingia katika Ukristo na njia ambayo ungeweza kuondolewa. Wakati mwingine hata alikula pamoja naye.

Kwa wale wasiojua mambo haya, mambo kama hayo yanaweza kudhaniwa kuwa upotovu wa kiakili na yasiwe na thamani kubwa zaidi kuliko mambo ya kuwaziwa tu. Lakini wale ambao wamepata uzoefu binafsi wa mambo kama hayo na wanaofahamu sana sayansi ya kiroho wanaweza kuyaelewa na kuyathamini kikamilifu. Hali hizi za kiroho ni tofauti kabisa na hali zinazotolewa na tahadhari


Ukurasa 08

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE







Maisha baada ya kifo

Makala hii iliandaliwa na Hazrat Khalifat ul Masih II[ra] na ikawasilishwa katika mkutano mkuu wa dini huko London na kuwa sehemu ya kitabu kiitwacho Ahmadiyyat yaani Haqiqii Islam.

Katika hatua zote hizi tatu mwanadamu hupata maumivu au raha kwa mujibu wa ukuaji wake wa kiroho, yaani, anatambua furaha ya peponi au mateso ya motoni hata katika kipindi chake cha ujauzito, kipindi chake cha uchanga na hatimaye baada ya ukuaji wake kamili; utambuzi wake pekee ndio wenye kasoro au ukamilifu kidogo wakati wa hatua mbili za awali, kuwa mkamilifu katika mwisho.

Katika hatua hii utambuzi wa mwanadamu wa raha na maumivu huwa mkamilifu, na hatua hii inaitwa peponi au motoni. Hatua hii haina mwisho.

Hakuna pazia kati ya kifo na hisia ya furaha au maumivu; nafsi pekee katika jitihada zake za kujirekebisha, na kujitayarisha kwa ajili ya, hali mpya za maisha



ya mwisho. Nafsi ya mwanadamu inaendelea kusonga mbele na kupita kutoka hatua moja hadi nyingine ya juu zaidi. Quran Tukufu inasema:

Ambao Malaika huwafisha hali wamejidhulumu nafsi zao. Basi watatoa amani (wakisema): Hatukuwa tukifanya uovu wo wote. Naam, hakika Mwenyezi Mungu Anajua sana mliyokuwa mkitenda. Kwa hiyo ingieni milango ya Jahanamu kwa kukaa humo. Basi ni baya sana kao la wafanyao kiburi.


Na wanaambiwa wale walioshika utawa: Ni nini Aliyoteremsha Mola wenu? Wanasema: Heri. Ama wale waliofanya wema katika dunia hii watapata wema, na hakika nyumba ya Akhera ni nzuri; na ni bora kabisa nyumba ya washikao utawa.

Bustani za milele wataziingia; inapita chini yake mito; humo watapata watakacho. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Awalipavyo washikao utawa. Wale ambao Malaika huwafisha wanapokuwa katika hali njema, watasema: Amani iwe juu yenu; ingieni Pepo sababu ya yale mliyokuwa mkiyatenda. (Q.16:v.29,30,33).

Mtukufu Mtume (sa) amesema, 'Kaburi linaweza kuwa bustani ya pepo au shimo la moto.'

Hii inaonyesha kwamba nafsi inaendelea katika hali ya uzima kwa muda wote, na huanza mara

HABARI UK> 11



Je, Wajua?

Gravity ni hali inayofanya kitu kimoja kivute kitu au vitu vingine kukielekea. Kila kitu kina gravity, Baadhi vina gravity kubwa kuliko vingine. Vyenye gravity kubwa huvuta vyenye ndogo. Mwanadamu na kila kilichopo ardhini huvutwa kuelekea chini ya dunia kwa sababu gravity imeshinda katika vita ya mvutano. Ndio maana huwezi kurusha jiwe likaelekea juu tu bila kurudi chini. Ukiruka pia lazima utarudi chini.

Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 3,000/=. (Tunaomba radhi kwa makosa yaliyojitokeza mwezi uliopita)

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com